**TANZANIA ASSEMBLIES OF GOD**

# MSIMAMO WA KANISA KUHUSU HALI YA USHOGA KWA MUJIBU WA NENO LA MUNGU

Miaka 13 ya Moto ya Uamsho!

Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya neema na uzima ambao anauachilia kwetu kila siku pasipo gharama yeyote tofauti na tamaduni zilizozoeleka kwamba hakuna kitu cha bure, lakini kwa Mungu wetu hutukirimia uhai na afya pasipo kutudai. Tunamtukuza sana Mungu wetu kwani kama Mtume Paulo anavyosema "Kwa maana ndani yake yeye (Mungu), tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu." Matendo 17:28

Kwa sasa nchi yetu na dunia kwa ujumla kumekuwa na wimbi la ajenda ya ushoga, usagaji, ndoa za jinsia moja na mambo yanayofanana na hayo. Mada hii imeleta mijadala mingi katika vyombo vya habari, kwenye taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali. Madhehebu mbalimbali duniani yamejaribu kujadili katika mitizamo ya aidha kukubali au kupinga jambo hili. Serikali yetu na jamii yetu imeonesha msimamo thabiti wa kupinga na kwa kuuelimisha umma juu ya upotofu wa jambo hili.

Pamoja na misimamo hii ya kupinga hali ya ushoga, usagaji na ndoa za jinsia moja, zimekuwapo dhana potofu za utetezi wa jambo hili katika mrengo wa Haki za binadamu na katika hali kuaminisha jamii kwamba watu huzaliwa na vinasaba ambavyo humsukuma mtu kuvutiwa na mtu wa jinsia yake.

Katika hali hii ya kuwepo kwa mitazamo mbalimbali kuhusu mapenzi na ndoa za jinsia moja, sisi kama kanisa la TANZANIA ASSEMBLIES OF GOD tunaona ni wakati muafaka wa kutoa fundisho la NENO LA MUNGU kuhusu mtazamo wa Mungu juu Ndoa. Mtazamo na msimamo wetu umejengwa katika tafsiri sahihi ya Neno la Mungu, ambalo ni MWONGOZO SAHIHI katika maisha ya UCHAJI MUNGU kama andiko lisemavyo "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema" (2Timotheo 3:16-17).

Katika mapitio ya Neno la Mungu hakuna fundisho la kibiblia linalohimiza ndoa za jinsia moja, ushoga au mtu kubadili jinsia kwa sababu ya uchaguzi wake. Wakati wowote Neno la Mungu lilipotumika kimakosa kutetea au kuhimiza mambo haya, ilitokana na tafsiri isiyo sahihi ya NENO LA MUNGU. Uchambuzi wa kina na tafsiri sahihi za Neno la Mungu, unatufikisha sisi kama Kanisa la TANZANIA ASSEMBLIES OF GOD tukisimamia Neno la Mungu hivyo tunatamka kwamba:

1. Ushoga ni dhambi na ni chukizo kwa sababu inakinzana na kanuni za mahusiano ya kijinsia ambayo Mungu aliyaasisi tangu mwanzo. Maandiko yanatuthibitishia kwamba Mungu alimuumba mwanamume na mwanamke kwa sura na mfano wake (Mwanzo 1:27). Ni baada ya uumbaji huu wa mwanadamu mwanamme na mwanadamu mwanamke anatoa amri ya kuzaa na kuongezeka.
    - Katika uumbaji wa mwanadamu alianzisha kanuni zinazotawala na kuongoza mahusiano ya kijinsia ambayo kutokana na hayo uzao wa mwanadamu ungeendelezwa.
    - Ni katika mfumo wa mahusiano ya jinsia tofauti ndipo tunapata muunganiko unaoleta maana kisaikolojia, unatengeneza mahusiano ambayo kwa asili yanakubalika na kuunda familia inayoanza na watoto wanaopatikana kupitia mahusiano ya kujamiiana mwanadamu mwanamme na mwanadamu mwanamke.
    - Mwanadamu anapoamua kuugeukia ushoga au usagaji anakuwa ameasi kanuni ya Mungu ya mahusiano ya jinsia tofauti ambayo aliyabainisha kwamba mwanaume atamuacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mke wake nao watakuwa mwili mmoja (Mwanzo 2:23-24).
    - Katika mafundisho na huduma ya Yesu alisisitiza kwamba, tangu mwanzo Mungu aliumba mtu mume na mtu mke, kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake na ataambatana na mkewe na hao wawili (Mume *-jinsia ya Kiume* na mke-*jinsia ya kike*) watakuwa mwili mmoja (Mathayo 19:4-6). Fundisho hili la Yesu ni MSISITIZO wa Agizo na Mpango wa Mungu kwa NDOA YA KIMUNGU KATI YA MWANAMME NA MWANAMKE.
2. Ushoga ni dhambi kwa kuwa neno la Mungu linatangaza kwamba ni uovu na ni machukizo.

Mungu katika mahusiano yake ya kiagano na watu wake, aliwatenga na kuwapa kanuni za kimaadili za kuwaongoza katika maisha ya kila siku. Moja ya sheria ya maadili ilihuisiana moja kwa moja na kukataza ushoga. Baadhi ya maandiko ni:

- Mambo ya Walawi 18:22, “Usilale na Mwanamme mfano wa kulala na mwanamke, ni machukizo”.
- Mambo ya Walawi 20:13, “Tena mtu mme akilala pamoja na mtu mme kama alalavyo na mtu mke, wote wawili wamefanya machukizo, hakika watauawa, damu yao itakuwa juu yao.”
    - Msisitizo huu umerudiwa kwa ubora zaidi katika Agano Jipya kupitia nyaraka za Mtume Paulo. Katika barua kwa Warumi 1:21-27 Mtume Paulo anahusianisha uovu wa wale waliomkataa Mungu uliambatana na dhambi ya ushoga na usagaji. Msisitizo mwingine wa Mtume Paulo kuhusiana na kupinga ushoga upo katika 1Wakorintho 6:9-10. Mji wa Korintho ulikuwa umegubikwa na ukengeufu wa kimaadili wa kila aina ikiwa ni pamoja na mapenzi ya jinsia moja. Mtume Paulo aliweka wazi msimamo wa neno la Mungu tangu agano la kale kwamba ushoga ni chukizo kwa Mungu na wale wote watendao dhambi hiyo pamoja na ukengeufu mwingine wa maadili wasingeurithi ufalme wa Mungu.

3. Ushoga ni dhambi ambayo husababisha hukumu ya Mungu
    - Katika Maandiko Matakatifu (Mwanzo 19:4-11, 24, 25) tunaukuta mji wa Sodoma na Gomora ambao wenyeji wake walijulikana kwa matendo ya ushoga na walikuwa waovu kiasi kwamba walikusudia kuwatenda vibaya wageni wa Lutu. Katika Mwanzo 19:5 katika tafsiri kwa lugha ya awali inathibitisha kwamba walimwambia Lutu awatoe wale wageni wake waliokuwa wanaume ili wawaingilie kinyume na maumbile. Mungu aliingilia kati na kuwapiga wenyeji kwa upofu na hivyo walishindwa kutimiza dhamira yao ya kuwaingilia wageni wa Lutu. Mungu aliuhukumu mji wa Sodoma na Gomora kwa ajili ya uovu wa kimadili ikiwa ni pamoja na tabia hii ya ushoga.
    - Hukumu ya Mungu kwa miji hii miwili inatumika kama kielelezo cha ghadhabu ya Mungu kwa matendo ya ukengeufu wa kimaadili unaohusu kujamiaana (2 Petro 2:6, Yuda 1:7). Kielelezo cha hukumu - kimetumika kama rejeo la onyo kali kwa ukengeufu wa ushoga
- Kitheolojia, ndoa ni agizo la Mungu, ambalo pia kimantiki hii linabeba dhana ya Mungu ya kuasisi ndoa ya jinsia mbili. “ZAENI MKAONGEZEKE NA KUIJAZA NCHI” Mwanzo 1:28.

  Agizo hili lilimfanya Mungu amuumbe mwanadamu (*Anthropos-Mankind-Man-Mtu-Adam*, maana yake mwanadamu) Mwanzo 5:1-2, katika mifumo miwili (*two forms*), mwanamke na mwanaume. Wote wawili pamoja ndio wanaofanya “MTU, *Anthropos-Mankind*.”

  AGIZO KUU LA KUIJAZA NCHI LILILOTOLEWA NA MUNGU KATIKA UUMBAJI LINAWEZEKANA TU KAMA NDOA YA KIKRISTO YA KIBIBLIA, YA MUME (*Mwanaume Mwanadamu*), NA MKE (*Mwanamke Mwanadamu)* LITAFUATWA. NDOA ZINGINE NJE YA HII YA KIBIBLIA NI UASI JUU YA MUNGU KWA AGIZO KUU ALILOLITOA.

4. NDOA ZA JINSIA MOJA Ni mkakati wa kishetani wa kuivuruga taasisi ya Ndoa, Familia, Kanisa na Jamii kwa ujumla. Kwa mujibu wa Neno la Mungu familia huanza na Ndoa ya mwanamme na Mwanamke. Familia huzaa jamii na kuunda kanisa. Kwa mwanamme kumwoa mwanamme mwenzake au mwanamke kuolewa na mwanamke mwenzake ni mpango unalenga kuharibu familia, jamii na kanisa.

   JUMLA KUU NI KWAMBA NDOA ZA NJISIA MOJA NI MGOMO WA MWANADAMU AKIUNGANA NA SHETANI KULIKATAA AGIZO LA MUNGU LA KUZAA NA KUIJAZA NCHI YA DUNIA NA KISHA KUIJAZA NCHI YA MBINGUNI.

KANISA LINAAMINI KWAMBA LIPO TUMAINI KATIKA YESU KWA MASHOGA NA WASAGAJI KUBADILIKA TABIA

Maandiko yanaweka wazi kwamba ushoga na usagaji ni dhambi na machukizo mbele za Mungu na kwamba hukumu ya Mungu haiepukiki kwa machukizo hayo. Hata hivyo kwenye ukengeufu

huu mkubwa wa kimaadili Maandiko yanathibitisha kwamba Mungu anaweza kuwasaidia wenye dhambi wote kubadilika ikiwa ni pamoja na mashoga na wasagaji.

Katika kanisa la Korintho walikuwepo watu ambao hapo awali walikuwa mashoga lakini baada ya kuwekwa huru mbali na nguvu ya dhambi kwa neema ya Mungu walirudi katika maisha ya kawaida kama Mungu alivyowaumba na kama alivyo wakusudia wawe (1 Wakorintho 6:11)

Maandiko yanathibitisha kwamba nguvu ya damu ya Yesu hutakasa dhambi na haina mpaka katika kusafisha dhambi kwa wale wanaoridhia na kufanywa upya (2 Wakorintho 5:17). Hakuna doa la dhambi ambalo damu ya Yesu haiwezi kuliondoa (1 Yohana 1:9). Yesu kristo ni mwanakondoo wa Mungu anayezichukua dhambi za ulimwengu (Yohana 1:29), tunaamini kwamba dhambi hiyo ni pamoja na ushoga, usagaji, ndoa za jinsia moja na matendo yanayofanana na hayo

Mpango wa Mungu wa wokovu upo sawa kwa watu wote. Endapo shoga anapenda kuokolewa kutoka katika nguvu ya dhambi ni lazima aende kwa Mungu katika namna ileile ambayo wenye dhambi wengine wanaitumia kumrudia Mungu, yaani toba na kumwamini Yesu. Tendo la kumrudia Mungu linahusisha toba na imani, kwa njia ya kumkubali Yesu kama Bwana na mwokozi. Wokovu ni badiliko la papo kwa hapo ambalo huendana na tendo la kutubu.

Tendo la kutubu linawakilisha na kumaanisha kubadili nia kwa kuacha dhambi na kumwendea Mungu. Mtu anayemgeukia Mungu ni lazima atambue hali yake ya dhambi na mitazamo inayokinzana na fundisho la NENO LA MUNGU. Kwa maana hiyo dhambi ya ushoga na usagaji zinasameheka kwa mujibu wa Neno la Mungu na hasa mtu aliyekwama katika dhambi hizo anapotambua na kuhitaji msaada wa Mungu wa wokovu (Matendo 16:30-31)

MTAZAMO WA KANISA

Kwa mapitio ya Neno la Mungu na mwongozo wa Roho Mtakatifu kanisa linasimama na Kweli ya NENO la MUNGU kwamba:

1. NDOA YA KIBIBLIA INAYOKUBALIKA NI NDOA KATI YA MWANAMME NA MWANAMKE.
2. NDOA YA JINSIA MOJA NI DHAMBI NA CHUKIZO MBELE ZA MUNGU.
3. NENO LA MUNGU HALIJARUHUSU MAHALI POPOTE KWAMBA Mwanadamu anaweza kubadilisha jinsia kulingana na anavyojisikia au utashi wake, au kusema kwamba anavinasaba vinavyomfanya kuvutiwa kimapenzi na mtu wa jinsia yake.
4. Kanisa lina fursa ya kutangaza habari njema za msamaha wa dhambi kwa wanaokubali ikiwa ni pamoja na wanaoteswa na ushoga na usagaji.
5. Kanisa lipo tayari kutoa msaada wa ushauri, maombezi na mafundisho ya Neno la Mungu kwa waathirika wa USHOGA NA USAGAJI ili warudi katika hali ya kawaida kama ilivyokuwa kwa wakazi wa mji wa Korintho ambapo waathirika wa ushoga walisaidiwa hata wakarudi katika hali yao ya kawaida kwa neema ya Mungu kupitia Neno, maombezi na ushauri. (1 Wakorintho 6: 9-11).

USHAURI KWA JAMII

1. Sheria zilizopo hazitoshelezi kushughulikia wimbi hili na Ushoga, Usagaji, ndoa za jinsia moja na vitendo vinavyoendana na matendo haya, Kwani matendo haya yamekuwa janga

kwa taifa, kwa kuathili jamii kimaadili, kupata ulemavu wa viungo/maumbile na kupoteza mwendelezo wa kizazi. Tunashauri Serikali ione uwezekano wa kuboresha na kusimamia vema sheria zinazoweza kupambana na janga hili.

2. Tunaishauri jamii kuanzia ngazi ya familia ishikamane kwa pamoja katika kukilinda kizazi chote dhidi ya mbinu mbalimbali zinazotumika kuwashawishi watu kuingia katika vitendo hivi viovu. Kila mzazi au mlezi arudi kwenye jukumu lake la malezi bora kuhakikisha kizazi hiki kinabaki salama.
3. Tunatoa wito kwa taasisi mbalimbali za kidini kupitia Imani zetu kukemea waziwazi na kufichua jitihada zozote wanazotaka kuzitumia maadui wa tamaduni na desturi zetu kuhalalisha ushoga, usagaji, ndoa za jinsia moja na matendo yanayofanana na hayo katika jamii yetu.
4. Tunalihimiza kanisa liongeze juhudi katika elimu ya Neno la Mungu mashuleni, kupeleka fundisho sahihi la kibiblia kuhusu ndoa na familia. Taasisi zetu zirudi kwenye huduma za mashuleni ili kukikomboa kizazi hiki na janga hili.

Imetolewa na:



Rev Joseph Gabriel Marwa

Katibu Mkuu Tanzania Assemblies of God,

Kwa Niaba ya Halmashauri Kuu ya

Kanisa la Tanzania Assemblies of God.